KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA
DAYOSISI YA KASKAZINI MAGHARIBI
CHUO CHA MAFUNZO YA KILIMO NA MIFUGO IGABIRO
S.L.P 212-MULEBA
Simu: 0769683119/0625914767/0683829718
Email: igabirotia@yahoo.com Tovuti: www.igabirotia.ac.tz

Tarehe: ……..

Bw/Bi: **……**

YAH**: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA CHUO CHA MAFUNZO YA KILIMO NA MIFUGO IGABIRO KWA NGAZI YA ASTASHAHADA MWAKA WA MASOMO 2019/2020**

Husika na somo lililopo hapo juu.

Chuo cha mafunzo ya Kilimo na Mifugo **Igabiro** kipo wilayani Muleba – Kagera.Kutoka Muleba mjini ni Kilometa 15 magharibi ukipitia barabara ya Nshamba. Na kutoka Nshamba kufika chuoni ni kilometa 3 kusini mwa Nshamba barabara ya kwenda Kabale upande wa kushoto kuna kibao kinachoonesha chuo kilipo.Chuo kinamilikiwa na **Kanisa La Kiinjili La Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Magharibi.**

Chuo kimesajiliwa na Baraza laTaifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) tangu mwaka 2014 kwa usajili wa namba (Cert.No.REG/ANE/018), Pia chuo kina ithibati.

NACTE pamoja na uongozi wa chuo cha mafunzo ya Kilimo na Mifugo **Igabiro** Muleba wanakupatia nafasi ya kupata mafunzo kwa ngazi ya **Astashahada.**

Chuo kitafunguliwa na masomo yataanza October, 2019.

Gharama za **mafunzo, bweni,chakula,matibabu na internet** kwa mwaka ni **Milioni moja laki nane na elfu arobaini tu** (1,840,000/=) , ambazo utazilipa kwa vipindi vitatu.

1. Malipo wakati wa kuripoti chuoni ni 840,000/=
2. Malipo awamu ya pili (Januari) ni Tsh 500,000/=
3. Malipo awamu ya tatu (Aprili) ni Tsh 500,000/=

NB: Vifaa na michango inayohitajika wakati wa usajili wa mwanachuo mara afikapo chuoni ni kama ifuatavyo;

i. Pasport size nne (4)
ii. Ream paper mbili (2) A4.
iii. Cheti cha kidato cha nne, sita na cheti cha kumaliza Astashahada.
iv. Cheti cha kuzaliwa (Birth certificate)
v. Cheti cha daktari(Medical certificate of fitness) fomu imeambatanishwa.
vi. Spring file mbili(02) .
vii. Fedha kiasi cha Tsh 18,000/= kwa ajiri ya kulipia T-shirt inayotumika wakati wa matukio mhimu uwapo chuoni (Inapatikana chuoni), pesa hii inalipwa chuoni kwa mhasibu.

Tafadhali lipa michango yote kwenye akaunti tajwa hapo chini kwani hatupokei pesa tasilimu, isipokuwa risiti ya benki (Bank pay in receipt)

(i) NBC – ELCT IGABIRO TRAINING INSTITUTE OF AGRICULTURE
A/C N0. 027103001001.
(ii) CRDB – ELCT IGABIRO TRAINING INSTITUTE OF AGRICULTURE
A/C N0. 0150216227000

4. Mahitaji mengine ni kama ifuatavyo;

(i) (a) Sare ya darasani kwa wanafunzi wa fani ya Agriculture Production;
- Suruali nyeusi na shati jeupe mikono mifupi au mirefu na viatu vyeusi au kahawia kwa wavulana.
- Sketi nyeusi ndefu na shati jeupe mikono mifupi au mirefu na viatu vyeusi au kahawia kwa wasichana.
- Ovalori na Gambuti kwa wanafunzi wote wakati wa mafunzo ya vitendo na mitihani.

(b) **Sare ya darasani kwa wanafunzi wa fani ya Animal Health and Production;**
- Suruali nyeusi na shati jeupe mikono mifupi au mirefu na viatu vyeusi au kahawia kwa wavulana.
- Sketi nyeusi ndefu na shati jeupe mikono mifupi au mirefu na viatu vyeusi au kahawia kwa wasichana.

- Ovalori na Gambuti kwa wanafunzi wote wakati wa mafunzo ya vitendo na mitihani (ni lazima)
-Laboratory white coat (ni lazima)

(ii) Vifaa vya darasani

(a)Kwa wanafunzi wa Agriculture and Production

- Wanafunzi wote wanatakiwa kuja na daftari/counter book nane(8) kwa semista, kalamu za risasi na wino, rula, kifutio mathematical set na pesa kwa ajili ya stationary na kujikimu.
- Kikokotozi (Scientific calculator).

(b) Kwa wanafunzi wa Animal Health and Production

- Wanafunzi wote wanatakiwa kuja na daftari/counter book nane(8) kwa semista, kalamu za risasi na wino, rula, kifutio mathematical set na pesa kwa ajili ya stationery na kujikimu.
- Kikokotozi (Scientific calculator).
- Thermometer (ni lazima)
- Stethescope (ni lazima)

(iii) Vifaa vya bwenini

-Mwanafunzi anatakiwa kuja na shuka mbili,blanket,chandarua na mto.

(iv) Vyombo vya kulia chakula

- Mwanafunzi anatakiwa aje na sahani,bakuli, kijiko na kikombe.

(v) Vifaa vya michezo

-Mwanafunzi anatakiwa aje na vifaa vya michezo kulingana na aina ya michezo anayopendelea.

(vi) Vifaa vya usafi

-Mwanafunzi anatakiwa aje na vifaa vya usafi wa mwili kama vile ndoo/beseni, mswaki, sabuni nk.

5. MUHIMU:-

Kwa wanafunzi wa **mwaka wa pili** kila mwanachuo anatakiwa kuwa na fedha ya somo la mazoezi kwa vitendo atakayoitumia akiwa nje ya chuo kwa mwezi mmoja . Fedha hiyo ni kati ya Tsh **200,000/=** hadi **350,000/=** kulingana na uwezo wa mzazi / mlezi / mwajiri kwa ajili ya chakula na malazi. Mazoezi ya vitendo yanafanyika mwanzoni mwanzoni mwa semista ya pili.

6. Mahali chuo kilipo

Chuo cha mafunzo ya Kilimo na Mifugo **Igabiro** kipo wilayani Muleba – Kagera. Kutoka Muleba mjini ni Kilometa 15 magharibi ukipitia barabara ya Nshamba. Na kutoka Nshamba kufika chuoni ni kilometa 3 kusini mwa Nshamba barabara ya kwenda Kabale upande wa kushoto kuna kibao kinachoonesha chuo kilipo.
Kutoka manisipaa ya Bukoba, pita barabara ya Bukoba –Muleba au Bukoba – Kamachumu kuja Nshamba.
Mara ufikapo chuoni, wasiliana na afisa udahili (Admission Officer) kwa usajili na malazi pamoja na huduma zingine mhimu.
Hakikisha unakabidhi fomu ya kujiunga na chuo(joining instruction) wakati wa usajili.Unatakiwa kuripoti chuoni mapema kama tarehe zinavyo elekeza, kushindwa kufanya hivyo inaweza kupelekea kupoteza nafasi hiyo.

7. Maelekezo ya jumla

- ✓ Masomo yako yatachukua mda wa miaka miliwi kwa ngazi ya Certificate (Astashahada) na mwaka mmoja kwa ngazi ya Diploma (Upgrading) na watu wa form six masomo yao ni miaka miwili ili kuhitimu Diploma katika fani ya Agriculture Production.
- ✓ Lipa ada na michango mingine kwa wakati sahihi ili kuepusha usumbufu kwa mwanafunzi na upande wa utawala.
- ✓ Ukiwa chuoni unatakiwa kuzingatia sheria za chuo kama zinavyoelekeza.
- ✓ Hakikisha umeweka utaratibu mzuri wa kazini kwako au nyumbani ili kuepusha ruhusa za mara kwa mara ambazo zitapelekea kupoteza vipindi vya darasani.
- ✓ Hakikisha unakuja na vyeti halali ili kuepusha usumbufu
- ✓ Tengeneza nakala ya fomu ya maelekezo ya kujiunga na umuachie mzazi au mlezi wako kwa ajili ya kurejea maelekezo yaliyomo kama vile utaratibu wa kulipa ada na michango mingine.

Karibu sana chuoni kwetu na ufurahie kujifunza.

Karibu sana chuoni kwetu na ufurahie kujifunza.

…….
Sahihi ya mwanafunzi na tarehe

……
Nivegila T.K.
PRINCIPAL

EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA
NORTH WERSTEN DIOCESE
IGABIRO TRAINING INSTITUTE OF AGRICUTURE

P. O.BOX 212-MULEBA,
TE 0754756028
Email: igabirotia@yahoo.com and **Website:** www.igabirotia.ac.tz

TO: The Medical Officer

……

……

1. Name……
2. Age ……
3. Weight ……
4. Blood Examination: Hemoglobin ……..
   Any abnormalities noted ……...
5. Stool Examination……..
6. Urinalysis…….
7. T.B. Test (if negative, was immunization given)
   ……
8. Eyes ……
9. Chest……
10. Abdominal Examination.……
11. Spleen ……

    Liver ……

12. Any clinic complaints not noted above ……

    Asthma …….

    Headache …….

Signature and stamp

(**Medical Officer)**